# Utata kuhusu Dhana na Chimbuko la Wahadimu katika Kisiwa cha Unguja

*Zainab Ali Iddi*

**Ikisiri**

*Lengo la makala haya ni kujadili utata wa dhana ya Wahadimu na chimbuko lao linaloibuka kutokana na mitazamo ya wataalamu mbalimbali. Data za makala haya zimepatikana kupitia usaili na majadiliano ya majopo ya wazungumzaji wa Kimakunduchi na Unguja na kujadili kwa muhtasari chimbuko la Wahadimu. Kwa muda mrefu dhana ya Wahadimu imekuwa ikijadiliwa kwa mitazamo tofautitofauti kama inavyobainishwa na wataalamu mbalimbali wakiwemo wanahistoria, wanaisimu na wanaethnoisimu. Ili kuweza kuielewa vyema dhana hiyo, ni vyema kwanza tukaelezea kwa muhtasari kuhusu maeneo ya Tumbatu na Makunduchi pamoja na wakazi wake.*

## 1.1 Tumbatu

Tumbatu ni miongoni mwa visiwa vikubwa vya Zanzibar; kina urefu wa kilomita saba na upana wa kilomita tatu. Kwa ujumla, kisiwa hiki kina ukubwa wa kilomita za mraba takribani 15.5. Kimasafa, kiko umbali wa kilomita 48 kutoka mjini Unguja na kilomita tatu kutoka Mkokotoni[1]. Kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 2012 kisiwa hiki kilikuwa na idadi ya watu wapatao 20,000. Kieneo, wakazi wa kisiwa hiki wamejigawa katika maeneo makuu mawili, yaani Jongowe ambayo iko upande wa kusini na Gomani ambayo iko katika welekeo wa Kaskazini. Wakazi wote wa Jongowe na Gomani hujulikana kuwa ni Watumbatu.

Mbali ya shughuli nyingine zinazofanywa kama vile kilimo na biashara, kisiwa hiki pia ni maarufu katika shughuli za uvuvi[1]. Kwa upande wa sherehe, Watumbatu wana mila ya kusherehekea *mwaka kogwa*. *Mwaka kogwa* ni sherehe maalumu ya kusherehekea mavuno ya kumaliza mwaka na kuukaribisha mwaka mpya[1]. Kwa mujibu wa maelezo ya watoa taarifa wa utafiti huu, shughuli hiyo ya *mwaka kogwa* katika Tumbatu huegemezwa zaidi kwenye imani za dini ya Kiislamu kama, vile kusoma maulidi na kukiombea dua kisiwa kiepukane na mabalaa.

## 1.2 Makunduchi

Kijiografia, Makunduchi imegawanyika katika sehemu kuu mbili; Kusini na Kaskazini. Wakazi wa pande hizi mbili wanatofautiana katika harakati zao za kila siku ambapo Kusini hujishughulisha zaidi na shughuli za kilimo. Mazao wanayolima ni mahindi, mtama, mbaazi, viazi vikuu, muhogo pamoja na kilimo cha minazi, kwa kutaja baadhi tu. Upande wa Kaskazini wakazi wake ni wavuvi zaidi, ijapokuwa shughuli za uvuvi wa uzio zinafanyika hata kwa wakazi wa Kusini. Kwa upande wa sherehe, Wamakunduchi, kama walivyo Watumbatu (taz§ 1.1) wana mila ya kusherehekea *mwaka kogwa*[1]. Kinyume na Watumbatu ambao sherehe zao hujiegemeza katika misimamo ya kidini (taz § 1.1), sherehe za *mwaka kogwa* za Wamakunduchi hujikita zaidi katika mambo ya mila mbalimbali kama vile; kupigana *magomba*, kula mkate maalumu, kuchoma moto kibanda na kuomba kwenye mzimu. Kama ilivyo kwa Watumbatu, sherehe hizo za *mwaka kogwa* pia huchukuliwa kama ni njia muhimu ya kuusafisha mji kuondokana na balaa na hivyo hufanya maombi maalumu kwa ajili ya kijiji, nchi na hata kwa watu binafsi pamoja na kutabiri mavuno ya mwaka mpya yatakuwaje. Mila hizi hufanywa kwa mpangilio na utaratibu maalumu wa matukio. Vilevile, sherehe hizo hufanyika katika muda maalumu unaopatikana kwa kufuata kalenda maalumu ya Wamakunduchi (taz. Iddi 2011:02). Inasemekana kwamba, *mwaka kogwa* wa Kimakunduchi huenda sanjara na *mwaka kogwa* wa Tumbatu lakini mara nyingi

hutangulia ule wa Makunduchi na kufuatiwa na wa Tumbatu.

Kama inavyoeleweka, kihistoria Zanzibar ilikuwa na ujio wa wageni (taz. Ingrams 1925; Gray 1955; Freeman-Grenville, 1962; Davidson, 1967; Sherrif 1987; Chami, 1994; Sendaro 1997 na Chami 2006) lakini inaelezwa kwamba Watumbatu na Wamakunduchi wana Ubantu zaidi kwa vile hawajaathiriwa na majilio na mwingiliano wa wageni waliofika Zanzibar, hasa Waarabu ambao waliwaathiri sana watu wa Unguja mjini kilugha na kiutamaduni (taz. Stigand 1915:26; Sengo, 1992; 75-76; Iddi, 2011: 36; Makame, 2012: 39). Ama kuhusu kaifa hiyo Sengo katika makala yake anaeleza:

> "... (Wamakunduchi) ni watu wanaotosheleza sifa zote za umwambao….. ambao wanaonekana kuumili Uafrika katika majumba yao, majenzi yao, makulaji yao, namna zao na lafidhi za lugha yao ya Kikae ambayo imeitawala wilaya nzima, kama ni tofauti za Jambiani, Paje, Kizimkazi, Muyuni na Kae kwenyewe, ni ndogo ndogo sana......"Lau wangekuwa wana dalili za ujio wa kigeni …. Kungeonekana vitu vya asili na majina ya kigeni na mengi yenye kufanana na lugha nyingine".

Maelezo hayo ya Sengo yanaonesha namna ambavyo Wamakunduchi walivyoamili mila na utamaduni wa Afrika ambao hauna athari kubwa itokanayo na majilio ya wageni kutoka nje ya bara la Afrika.

### 1.3 Watumbatu na Wamakunduchi ni Wahadimu?

Baadhi ya waandishi wa zamani (taz. k.m Sacleux, (1909; Stigand, 1915; na Johnston, 1922) wanakubaliwa kuwa lugha za Kitumbatu na Kimakunduchi zinaitwa Kihadimu. Katika kulithibitisha jambo hili, kama tulivyokwishaona, pengine ndio maana maelezo ya wataalamu hao yanafanana na kukubaliana. Kwanza, wote wanasema kuwa Kitumbatu na Kimakunduchi ni Kihadimu. Pili, "lugha" hizi ni lahaja moja tu na sio mbili (jambo ambalo linaonesha kwamba huenda hawa watu ni wamoja ijapokuwa Wamakunduchi wako Kusini na Watumbatu wako Kaskazini). Tatu, Wahadimu ni watu wa mwanzo kuishi Zanzibar.

Tukiangalia kwa makini kufanana na kukubaliana kwa hoja za waandishi hawa inawezekana ikawa si kwa bahati mbaya bali ni kutokana na waandishi waliofuatia maandishi ya watangulizi wao; Stigand na Johnston kukubaliana moja kwa moja na maandiko ya mtangulizi wao Sacleux ambaye aliangalia kijuujuu tu kuhusu Kitumbatu na Kimakunduchi na kuibuka na hitimisho hilo pasi na kufanya utafiti wa kina. Aidha, kuna uwezekano mkubwa wa Stigand na Johnston kutofanya utafiti wa kina na badala yake wakayachukulia na kukubaliana, pasi na kuyasaili maelezo ya Sacleux; na huenda hii ikawa ndio sababu ya maandiko yao kutokuwa na maelezo ya kutosha katika kuthibitisha hoja zao. Kwa bahati mbaya, hata baadhi ya waandishi pia walifuata nyayo za waandishi hao wageni na kukubaliana na maelezo yao bila ya kufanya tafiti za kina. Ingawa ni muhimu na ni vyema sana kuangalia maelezo na hoja za waandishi waliotangulia lakini katika kufanya hivyo siku zote huhitaji uchunguzi zaidi. Tukiangalia maelezo ya Sacleux, Stigand na Johston tunabaini kuwa  hawakufanya utafiti wa kina bali waliandika kwa ufupi tu kuhusu watu na "lugha" zao.

Maelezo ya Sacleux, Stigand na Johnston yanatuambia mambo mawili; kwanza, Kimakunduchi na Kitumbatu ni lahaja moja. Pili, "lahaja" hiyo inazungumzwa kusini na kaskazini Unguja

ambapo kwa pamoja inaitwa Kihadimu. Kwa bahati mbaya kama tulivyokwishasema, waandishi hawa hawakufanya tafiti za kina zinazoweza kuthibitisha kama Kitumbatu ni sawa na Kimakunduchi.

**2.0 Utata kuhusu Dhana na Chimbuko la Wahadimu**

Dhana ya Wahadimu imebainishwa na kujadiliwa na waandishi na wataalamu mbalimbali katika mitazamo tofautitofauti. Kuna kundi lililowanasibisha Wahadimu na watumwa. Kundi la pili linasema kwamba, jina la 'Hadimu' lina utata kutokana na kutafsiriwa visivyo. Kundi la tatu, ni lile linaloona kuwa Wahadimu ni wenyeji wa asili. Kundi jingine ni lile ambalo linasema kwamba neno Wahadimu lilianza wakati wa Wareno.

Tukianza na kundi la mwanzo, wataalamu waliosema kwamba Wahadimu ni watumwa ni Sacleux (1909), Stigand (1915), Johnston (1922, 1939) na Gray (1977). Kwa mujibu wa maelezo yao, wanaeleza kwamba 'Wahadimu' wanapatikana Kusini na Kaskazini ya kisiwa cha Unguja. Sacleux (1909) alikuwa Mmisionari Mkatoliki wa kwanza kugusia kuhusu Wahadimu lakini hakutoa ufafanuzi wa kina zaidi ya kusema kuwa wanapatikana Kusini na Kaskazini ya Unguja.

Katika maelezo yake Stigand (1915: 25-26) anaeleza kuwa, Wahadimu ndio watu wa mwanzo wa asili kufika na kuishi Zanzibar kabla ya kuja kwa Waarabu. Hata hivyo, hakutoa maelezo ya kina kuhusu hao Wahadimu kama walitokea wapi, wana sifa au utamaduni wa aina gani na pengine wanakadiriwa kufika katika kisiwa cha Unguja katika karne ya ngapi. Hoja hii ya Stigand ni ya msingi lakini imekosa mashiko kwa vile imezungumziwa kwa juu juu tu bila ya ushahidi wa kina, hasa ikizingatiwa kuwa kuna maelezo kuwa neno Hadimu halikuwapo hapo mwanzoni bali lililetwa na Waarabu (taz. Knappert, 1992: 16; na Hans (2014: 04. Kama kwamba hiyo haitoshi, inavyoeleweka ni kwamba, kabla ya kuja wageni Zanzibar kulikuwa na wenyeji ambao walikuwa wametamakani katika karne nyingi zilizopita. Katika kundi hili, mtaalamu mwingine ni Johnston (1922: 39), ambaye katika kuwaeleza Wahadimu anasema kuwa:

> "Wahadimu ni miongoni mwa wakazi wa asili wa Zanzibar ambao kwa sasa wanaishi zaidi katika maeneo ya Kaskazini na Kusini mwa Kisiwa cha Unguja."

Akifafanua zaidi, Johnston (1922:39) katika kitabu chake cha *A Comparative Study of the Bantu and Semi- Bantu Languages* anaeleza kuwa Wahadimu ndio *Wanegro* wa awali kufika Zanzibar ambapo neno "Hadimu" linatokana na Waarabu na lina maana ya "watumishi". Maelezo ya Johnston yanatuambia kuwa Wahadimu ndio watu wa asili, wanaoishi Kusini na Kaskazini Unguja.

Tukiangalia vyema maelezo ya wataalamu wa kundi hili tutabaini kwamba kuna mkanganyiko wa mawazo na maelezo yao kutokana hoja yao kujengeka katika mitazamo miwili mikuu, nayo ni Wahadimu ni wenyeji wa asili na Wahadimu ni watumwa. Mitazamo hii kwa pamoja imezua mkanganyiko. Kwanza, kuhusiana na neno "Hadimu" ambalo kwa mujibu wa etimolojia ya neno na pia kwa wataalamu mbalimbali, neno hili hapo awali lilikuwa halipo lakini lililetwa walipokuja Waarabu katika visiwa vya Zanzibar (taz. Knappert, 1992: 16; na Hans, 2014: 04). Pili, madai kwamba Wahadimu ni wenyeji wa asili nayo yanahitaji uchunguzi zaidi hasa kutokana na kuhusishwa wenyeji hao wa asili na neno Wahadimu. Labda tujiulize inakuwaje wenyeji wa asili wa Zanzibar kuitwa Wahadimu ilhali neno 'Hadimu' lilikuwa haliwapo hapo awali; na kwamba neno hilo lililetwa na kuanza kutumika katika kipindi cha Waarabu (taz. Prins

1967:18).

Kwa mujibu wa historia Waarabu walifika katika visiwa vya Zanzibar kwenye karne ya 18, hali ya kuwa inasemekana kwamba wakazi wa mwanzo katika upwa wa Afrika Mashariki na visiwa vyake walikuwa wametamakani kabla ya kuzaliwa Kristo (taz. Gray, 1962: 11; Massamba, 2017:117-118). Kama kwamba hiyo haitoshi, utafiti wa kiakolojia uliofanyika Zanzibar (taz. Chami, 2005; Sinclair, Juma na Chami, 2006, 2007) uligundua kwamba Kusini Mashariki mwa Zanzibar waliishi binaadamu kwa maelfu ya miaka. Maelezo haya, yanaonesha kuwa katika visiwa vya Zanzibar watu waliishi katika karne nyingi sana zilizopita kabla ya kuja Waarabu ambao inasemekana kuwa huenda labda ndio walileta Uhadimu kwa maana ya utumwa (taz. Gray, 1955). Katika muktadha huu, madai ya kuwa Wahadimu ndio wenyeji wa asili wa visiwa hivi yanatia wasiwasi na ndio uliozua maswali; iweje neno lije mwisho baada ya karne kupita na miji kujengeka lakini jina hilo ndilo liwe jina la asili la wenyeji?

> Gray (1955), akinukuliwa na Madumulla (1995:46) anasema kwamba:
> “Wahadimu ni jina lililotoka kwa Waarabu kwa maana ya “watumwa”... ni jina ambalo halipendwi, ndiyo maana wanajiita Washirazi. Na ikiwa wanajiita Washirazi maana yake wanadai kuwa chimbuko lao ni Uajemi au mahala pengine nje ya Afrika, hususan Uarabuni, si geni katika historia ya watu wa pwani ya Afrika Mashariki....... Nionavyo mimi hata hivyo hawa ni watu mchanganyiko kutoka mrima (bara). Pia.... watu hawa hawajapata kupigwa vitani wala kufanywa watumwa. Ijapokuwa, kama wenyeji wengine wa Zanzibar, walitumikishwa katika mashamba ya karafuu”.

Kinyume na watangulizi wa awali, Gray anasema kuwa Wahadimu wametafsiriwa kuwa ni “watumwa”, lakini kwa mtazamo wake hao wanaoitwa Wahadimu, anasema kwamba hawajawahi kuwa wala kufanywa watumwa. Hata hivyo, akiendelea kufafanua anaeleza kwamba Wahadimu hawakuwa wenyeji wa Zanzibar bali walikuja kutoka Mrima na kuungana na wenyeji katika kufanya kazi za mashambani. Tukichunguza kwa makini maelezo ya Gray tunabaini kwamba katika kipindi hicho, watu wote waliokuwa wakifanya kazi mashambani walikuwa wakijulikana kama Wahadimu. Maelezo haya yanatuonesha kwamba jina Wahadimu halikuwa moja kwa moja linawahusu Watumbatu na Wamakunduchi tu.

Prins (1967:18-19) anakubaliana na hoja inayosema kuwa, Wahadimu ndio wakazi wa asili wa visiwa hivi ijapokuwa anaeleza kuwa, kundi hilo la Wahadimu ni mchanganyiko wa watu kutoka sehemu mbalimbali kama vile kisiwa cha Mayote na Segeju. Akifafanua zaidi anasema kwamba watu wamejikita katika maeneo ya Kusini Unguja (kwa maana ya Makunduchi na sehemu zake za karibu) kama vile Chwaka, Bwejuu, Makunduchi, Kizimkazi, pamoja na kisiwa cha Uzi kilichoko Mashariki. Ama kuhusu Watumbatu, Prins amewabainisha kama Washirazi. Kinyume na watangulizi wake katika kundi hili linalodai kuwa wahadimu ndio wenyeji wa asili; Prins hakubaliani na mtazamo wa Wahadimu kuwa ni watumwa na hivyo hakuwanasibisha Wahadimu na utumwa bali zaidi alisema kwamba walikuwa ni vijakazi na watwana; anasema:

> “Asili ya watu wa Zanzibar inatokana na mchanganyiko wa watu kutoka sehemu mbalimbali, wakiwamo Wahadimu, waliokuwa wajakazi na watwana na si watumwa, ambao mara chache huchukuliwa ndio wenyeji wa visiwa hivi na hivyo ni mara chache kuhusishwa kuwa ni wageni kutoka nje. Prins (1967: 18).

Kundi jingine ni lile linalosema kwamba neno 'Wahadimu' limetafsiriwa kimakosa kinyume na asili yake lilivyo, tafsiri ambayo imesababisha kupatikana kwa dhana ya utumwa; jambo ambalo si sahihi. Ndio maana kutokana na kutafsiriwa huko vibaya kwa jina hili la Kihadimu, baadhi ya wakazi katika jamii hizo walianza kujisikia vibaya kuendelea kujiita Wahadimu na hapo ndio wakaanza kujiita Washirazi au kwa majina yao ya Kimaeneo (taz. Gray, 1967; Massamba, 2007). Wafuasi wa kundi hili ni Knappert (1992), Graya (1955) na Prins (1967). Kwa mujibu wa Prins, Wahadimu sio watumwa bali ni manokoa. Ama kuhusu kaifa hii Knappert (1992:17) anaeleza:

> *"The settlers from the Middle East refer to the African population of Zanzibar as khadimu (from Arab khadim), a word usually but incorrectly translated as servants, the correct derivation is from Arab. Qadim "old people" the qadim (to be that spelt) are the "people of old". The Arab consonants kh and q are often confused by Swahili speakers. The kadimu live today in all parts of Zanzibar Island but in the east and south lived exclusively on the western side of the island".*
>
> "Wahamiaji kutoka Mashariki ya Kati waliwachukulia jamii ya Waafrika wote wa Zanzibar kuwa ni Wahadimu (kutokana na jina la Kiarabu Khadim). Jina hili kinyume na kawaida yake lilitafsiriwa kimakosa kwa maana ya mtumishi (mtu anayemtumikia mtu mwingine), tafsiri sahihi kutoka Kiarabu ya neno Qadim ni "watu wa zamani au wa kale". ….. Kwa sasa Wahadimu wanaishi au kupatikana katika maeneo yote ya Zanzibar, Mashariki na Kusini lakini zaidi wamejikita katika upande wa Magharibi ya kisiwa hiki" (1992:17).

Maelezo ya Knappert na Prins yanaonesha kuwa, kuna mkanganyiko wa tafsiri ya neno 'hadimu' ambalo wengine walilichukulia kama ni watumishi (watumwa), wengine kama Waafrika wa Zanzibar na wengine kama wakazi wenye kipato cha chini ambao walikuwa wanategemea kufanya kazi kwa matajiri ili waweze kuendesha maisha yao. Kwa mujibu wa maelezo yao, inaonekana kwamba mkanganyiko wa neno Wahadimu umechangiwa sana na watawala waliofika Zanzibar ambao kwa sababu zao za kisiasa na utashi wao wa madaraka waliwabeza wenyeji na kuwapa majina yasiyofaa ili kuweza kuendeleza tawala zao na kuonesha tofauti zilizopo baina yao na wanajamii, kwa maana ya mtawala na mtawaliwa, na ndio maana Knapert akasema kuwa wahamiaji karibu wote kutoka Mashariki ya Kati waliwaita wakazi wa Zanzibar kuwa ni Wahadimu (taz. Abdulaziz (1979) na Knappert 1992:17). Kama kwamba hiyo haitoshi, akisisitiza hoja yake kuwa Wahadimu si watumwa kama walivyotafsiriwa, Knappert anazidi kueleza kwamba:

> *"…... As we have already seen they were the Wakadimu "old people", not Wahadimu "servants", as the Arabs unjustly called them. Knappert (1992:27)*
> *"…… Kama tulivyokwishaona kwamba watu hao ni Wakhadimu kwa maana ya kuwa ni "watu wa kale" na sio Wahadimu kwamba ni watumwa, ambapo Waarabu hawakuwatendea haki kuwaita hivyo. Kwa vile wao si watumwa….." (1992:27).*

Hoja ya Knappert kwa kiasi fulani iliungwa mkono na Madumulla (1995:47) na anasema:

> "Inaelekea kuwa wataalamu kadhaa walioandika kuhusu Wahadimu walilipata jina hilo, ama kutoka kwa watu ambao si Wamakunduchi au

> kutoka vitabuni. Kuendelea kuwaita Wahadimu si kuwatendea haki, bali ni kuzidi kuuakisi utwana wao chini ya Mwarabu".

Kwa ujumla maelezo ya Knappert yanadhihirisha wazi utata uliopo kutokana na waandishi na wataalamu kutofautiana kimtazamo juu ya dhana hii ya Wahadimu. Aidha, maelezo ya Knappert yanaonesha pia kuwa, inawezekana huenda kabla ya kuja wageni na baadaye kwa watawala na dhana yao ya Wahadimu kulikuwa na wenyeji waliokuwa wametamakani, jambo linalodhihirisha kuwa huenda labda uhadimu ulikuja baadaye, pengine kwa sababu za utawala na kisiasa (taz. Gray 1955, Freeman –Grenville 1962, Ingram 1966, Davidson 1967, Sherrif 1987, Chami 1994, Sendaro 1997, Chami 2006).

Mbali ya makundi hayo mawili, kundi jingine lililojitokeza na dhana hii ya Wahadimu ni kama asemavyo Hans (2014) kwamba Wahadimu walipatikana baada ya kuja kwa Waarabu katika visiwa vya Unguja ambapo Wahadimu hao walikuwa ni watumishi. Pili, Wahadimu ni wenyeji wa asili wa visiwa vya Zanzibar katika maeneo ya Kusini na Kaskazini Unguja hasa katika kisiwa cha Tumbatu. Tatu, kabla ya Wahadimu kulikuwa na watu wanaojulikana kama watu wa Kae ambao hao kuna uwezekano mkubwa kuwa ndio watu wa asili wa maeneo hayo. Nne, jina la Wamakunduchi limekuja katika miaka ya hivi karibuni na hivyo jina la asili ni Wahadimu. Kama kwamba hiyo haitoshi, akifafanua zaidi katika makala yake *"Asili na Chimbuko la Wazungumzaji wa Kimakunduchi"* anasema kuwa, licha ya matumizi ya jina la Kihadimu kuhusishwa zaidi na wageni na wakati mwingine kuhusishwa na dhana ya utumwa, jina hili lilikuwa likitumiwa pia na wakazi wa Kusini Unguja kwa maana ya lugha ya wakazi wa eneo hilo ambao hawajaathiriwa na ujio wa wageni (taz. 63-64).

Maelezo ya hapo juu yanaungwa mkono na maelezo yafuatayo:

> "…. Kuna uwezekano kwamba jina hili (Wahadimu) lilianza kutumiwa na Waarabu kwa sababu hata asili yake ni Kiarabu". Kuna uwezekano pia kwamba watumishi wengi waliokuwa wakiwahudumia Waarabu walitoka maeneo ya Kusini na baadhi maeneo ya kaskazini mwa kisiwa cha Unguja hasa katika kisiwa kidogo cha Tumbatu". Tukumbuke kwamba Waarabu wengi waliishi zaidi maeneo ya mjini na pengine isingekuwa rahisi kupata watumishi wazuri maeneo hayo. Kama hivyo ndivyo, ndiyo maana jina la Wahadimu lilitumiwa kwa maana ya wakazi wa kusini Unguja na kwa kiasi fulani wakazi wa Kaskazini mwa kisiwa cha Unguja hasa kutoka katika kisiwa cha Tumbatu. … Kwa watawala wapya jina la Kihadimu lilihusishwa zaidi na utabaka kwani kusema kwamba neno hadimu ni mtu anayemtumikia mtu mwingine, maana yake ni kwamba kulikuwa na kundi la watu wanaotumikiwa na kundi jingine la watu wanaowatumikia watu hao. Hivyo matumizi ya jina la Kihadimu yakaanza kufifia….. Imebainika kwamba jina la Kikae ndilo jina la asili la lugha ya watu wa kusini Unguja ambao pengine ndilo lililokuwa likitumika hata kabla ya jina la Kihadimu lililoletwa na Waarabu. Hadi sasa wakazi wa Kusini Unguja wanapendelea kujiita Wakae (2014:64-65).

Uwezekano alioueleza Hans hapo juu unatuonesha kwamba; neno Hadimu asili yake linatokana na Waarabu na hivyo matumizi yake yalianza katika kipindi hicho cha Waarabu na hivyo hata hao Wahadimu walianza kupatikana baada ya kuja kwa Waarabu ambapo harakati za utumwa ndipo ziliposhamiri. Kwa upande mwengine, anatueleza kwamba Watumbatu na Wamakunduchi

ndio walikuwa watumishi waliokuwa wakitumi- kishwa na Waarabu. Hoja ya kuwa Watumbatu na Wamakunduchi walipata jina kwa sababu tu ni wakazi wa maeneo hayo ndipo wakawa watumishi ambao walikuwa wakichukuliwa kwa ajili ya kufanya kazi za Waarabu kwa wakati huo, yanahitaji kufanyiwa kazi na kuchunguzwa zaidi. Hii ni kwa sababu, kabla ya kuja Waarabu wakazi hawa walikuwa na maeneo yao Kusini na Kaskazini Unguja, hivyo bila shaka walikuwa na mambo yao kamili yaliyotimia kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Kuja watu kutoka mbali na kuwafanyisha kazi tu na kuweza kuwabadilisha hata asili yao ni jambo linalohitaji tafakuri ya kina.

Aidha, katika dondoo hilo hapo juu, kuna hoja zinazopingana; moja inasema kuwa dhana ya Wahadimu ililetwa na Waarabu, na hoja ya pili ni kwamba Wahadimu ni Wamakunduchi na Watumbatu ambao ndio wenyeji wa asili ambao hawajaathiriwa na wageni na hivyo jina la Kae ndio la mwanzo na la asili la watu wa Kusini Unguja na ambalo pengine ndilo lililokuwa likitumika hata kabla ya jina la ‘Wahadimu’ lililoletwa na Waarabu. Sasa tujiulize ikiwa wenyeji hawajaathiriwa na wageni, ilikuwaje wakaweza kuupata huu uhadimu? Hali ya kuwa na uhadimu ulikuja na kuletwa na Waarabu, katika kipindi ambacho hata Hans mwenyewe anakiri kuwa wenyeji wa asili walikuwako na ambao baadaye wakawa Wahadimu? Aidha, bado anahoji kama kweli jina la Wahadimu halikuweko mwanzoni, kwa nini waandishi wa zamani walitaja jina hili na wasilitaje jina la watu wa Kae? Ama kwa hakika, huu ni mkanganyiko ulio dhahiri kabisa ambao umekosa msimamo thabiti na hivyo bado unahitaji kuchunguzwa na kufafanuliwa zaidi. Ikumbukwe kuwa hoja ya kuwahusisha wageni au waandishi wa awali kutumia jina la Wahadimu inaweza kuwa nyepesi kwani haina mashiko hasa tukizingatia kuwa waandishi hao kwanza walikuwa ni wageni. Pia, hawakufanya utafiti wa kina ambao ungetuonesha hao Wahadimu; hivyo basi, hawana data zinazoweza kuthibitisha hoja zao. Matumizi ya neno Wahadimu/Kihadimu kwa wageni yanaweza kusababishwa pia hata na sababu za kiutawala kwa wakati huo ambapo waandishi hao walikuwa katika kundi la watawala. Kwa upande mwingine, mara nyingi katika jamii, lugha ya watawala au wenyeji ndio inayotumika. Swali la kujiuliza ni kwamba je, mtumwa ana lugha? Inakuwaje mtumwa aingie pahala na kuhodhi eneo kiasi cha kubadilisha lugha ya wanajamii walio wengi? Ijapokuwa nadharia za lugha zinabainisha kwamba lugha huweza kupata mabadiliko na hata kupoteza uasili wake lakini wingi wa watumiaji na maingiliano yao ni muhimu, ambapo kwa vyovyote watumishi walioletwa kutoka mbali au waliochukuliwa na kuhama hama kutoka maeneo yao ya asili wasingeweza kuwa wengi kuliko wenyeji wakaweza kuhodhi lugha hadi kuibadilisha. Kuhusu kaifa hii, Sengo (1992: 78) anasema:

> “Lugha ya Kihadimu haipo. Hakuna lugha inayowanyanyasa wenye lugha. Kihadimu ni “kisaidizi” au lugha ya watumishi/wasaidizi. ...... Lugha ya wilaya ya kusini ni Kikae”.

Aidha, kihistoria inajulikana kwamba kisiwa cha Tumbatu ni miongoni mwa miji ya awali ya wakazi wa visiwa vya Unguja na Pemba na baadaye watu wakaweza kutawanyika katika maeneo mbalimbali yakiwemo ya watu wa sehemu za Nganani, Makunduchi na Mkoani Pemba. Pia, ni sehemu iliyokuwa na utawala wake wakati wa utawala wa jadi wa Mwana wa Mwana. Kama hivi ndivyo, bila shaka watu wa sehemu hizi walistaarabika mapema kulinganisha na sehemu nyingine, iweje leo ndio wakubali kuwa watumishi kirahisi rahisi tu? Isitoshe, inasemekana kwamba wakati wa Waarabu watumishi walikuwa wametapakaa kila pahala kwa mujibu wa mahitaji ya watawala na ndio maana kukawa kuna biashara ya utumwa, sasa sijui hawa

wanaoitwa Wahadimu kama ni hao watumwa walioletwa katika karne ya 18 kutokana na biashara ya utumwa au ni wale wenyeji wa asili katika maeneo ya Kusini na Kaskazini mwa Unguja katika kisiwa cha Tumbatu? Vilevile, tukiangalia maumbile ya kisiwa cha Tumbatu, tutaona kuwa wakazi wa maeneo hayo tokea hapo awali si wakulima bali ni wavuvi kutokana na maumbile ya eneo lao. Sasa tukirejelea dondoo yetu hapo juu kuwa, Waarabu waliwachukua Watumbatu kwa sababu ya kupata watumishi wazuri yanatia wasiwasi. Ikumbukwe kwamba, si kisiwa cha Tumbatu tu na Makunduchi, bali katika kipindi hicho Zanzibar yote ilikuwa imetawaliwa, hivyo basi kuna shaka kidogo kukubaliana na hoja kwamba watumishi walichukuliwa kutoka sehemu hizo mbili tu na ndio maana wakaitwa Wahadimu! Kama tulivyoona, kwa mujibu wa Knappert, Waarabu waliwachukulia Waafrika wote walioishi Zanzibar kama Wahadimu, iweje leo iwe kwa Wamakuduchi na Watumbatu tu? Wasiwasi wa hoja hii unapata mashiko zaidi kutokana na baadhi ya wataalamu kudai kwamba; hakuna historia inayoonesha kuwa maeneo hayo yalikuwa ya watumwa hasa ikizingatiwa kwamba hayo ni maeneo ya miji ya mwanzo ya Zanzibar (taz. Gray, 1977; Knappert, 1992; Sengo, 1992).

Iwapo tunaona kwamba hoja za kina Knappert na *wenzake* zina mashiko, basi dhana ya kuwa, watumishi walikuwa wakitoka sehemu moja tu nayo pia inatia shaka, kwani historia inaonesha kwamba Zanzibar kulikuwa na biashara ya watumwa ambao walikuwa na kazi zao za kilimo, tujiulize waliokuwa watumishi hasa walikuwa ni watu gani? Ni hao watu ambao ni pamoja na Wamakunduchi na Watumbatu tu? Au walikuwa kutoka sehemu mbalimbali ndani na nje ya Zanzibar ambapo baadhi yao waliletwa kama watumwa kutoka nje ya Zanzibar, na ambao waliweza kusambaa katika maeneo mbalimbali ya mjini na shamba katika kisiwa cha Unguja.

Kwa mujibu wa watoa taarifa wetu hata ndani ya kijiji cha Makunduchi, baadhi ya wakazi wake waliweza kuwachukua na kuwaajiri watumishi kwa ajili ya kufanya kazi za kilimo na kulea watoto, jambo linalothibitisha kwamba si Waarabu tu ndio walikuwa na watumishi bali hata wenyeji wa Makunduchi kwa wakati huo waliweza kuwa na watumishi. Kama hivi ndivyo, madai kuwa wao ndio walikuwa watumishi tu yanatia shaka. Historia inatueleza kwamba, kisiwa cha Tumbatu ni miongoni mwa miji ya mwanzo ya Zanzibar ambayo inasemekana kuwa, ilikuwa na dola ya utawala kamili yenye nguvu; utawala huo ukijulikana kama Mwana wa Mwana katika enzi hizo. Kama hivi ndivyo, bila ya shaka itakuwa sehemu hiyo ilikuwa ni muhimu katika uchumi na maendeleo ya visiwa hivi na hivyo si rahisi kukubaliana na hoja ya kwamba sehemu hiyo ndio ilikuwa kitovu cha watumwa au watumishi kwa wakati huo.

Ama kwa hakika, maelezo ya Hans bado yana utata na hayako wazi na si vibaya kusema yanazongana kutokana na kujirudia rudia na kukosa jibu au msimamo mmoja kuhusiana na Wahadimu, kwa vile mitazamo yake inasigana yenyewe kwa yenyewe. Aidha, maelezo ya Hans hayakuweza kujibu hoja ya Wahadimu bali kwa maoni yetu yameongeza na kupanua zaidi tatizo la dhana ya Wahadimu katika kuhusishwa na Kitumbatu na Kimakunduchi pamoja na utumwa. Hali hii inadhihirisha kwamba bado kuna utata na hivyo tafiti za kina zinahitajika ili kuziba mapengo yaliyopo juu ya dhana hii ya Wahadimu.

Kama kwamba hiyo haitoshi, akitoa maoni yake katika kuunga mkono hoja ya Wahadimu, Hans (2014: 04-05) anasema kwamba:

> "Ukiyapitia maandiko mengi yanayohusu lahaja za Kiswahili, utaona kwamba jina la Kimakunduchi limeanza kutumika mwishoni mwa miaka ya 1970. Hata hivyo, kwa sasa Kimakunduchi na Kikae hutumiwa kama majina mbadala"

Ni dhahiri kwamba, fikra ya kwamba neno Kimakunduchi ambalo bila ya shaka linatokana na jina la wakazi wake Wamakunduchi kuwa ni jipya, limekuja hivi karibuni iko wazi. Hata hivyo, katika kufafanua asili ya kupatikana kwa jina Makunduchi, Hans (2014:65-67) anasema kwamba; kwanza jina hili linatokana na ujio wa watu kutoka Kunduchi. Pili, jina hili linasemekana kwamba linatumiwa zaidi na watawala na watu waishio nje ya Makunduchi. Tatu, jina hili limepata umaarufu kutokana na nguvu ya kisiasa. Makala haya hayapingi hoja ya uwezekano wa kupatikana jina la pahala kutokana na ujio wa watu katika sehemu hiyo, na hivyo hoja ya ujio wa watu kutoka Kunduchi kuwa ndio asili ya jina la Wamakunduchi ina mashiko. Hata hivyo, ni vyema ifahamike kwamba; ujio wa watu katika upwa wa Afrika Mashariki ambao wametajwa kama Wahadimu, Wamakunduchi na Watumbatu kwa kutaja baadhi tu, katika miaka ya sabini (1970) ulikuwa umeshakoma. Aidha, hoja ya nguvu za kisiasa ingewezekana kuwa na uzito ikiwa mwandishi angetuonesha na kubainisha umuhimu wa eneo hilo kisiasa au hata kihistoria. Ama kwa hakika kushindwa kujiegemeza katika hoja moja kunaonesha kuwa maelezo ya Hans yanahitaji kuchunguzwa zaidi hasa ikizingatiwa kuwa yanajirudia rudia na hayako wazi.

Naye Ingrams (1924) anaeleza tu kuhusu Wahadimu kwamba; ni watu wa Kusini Unguja. Hata hivyo katika tafiti zake pamoja na kueleza sifa mbalimbali za upekee za watu wa Kusini hakuhusisha suala la Wahadimu na utumwa. Mbali ya Ingrams, baadhi ya waandishi nao pia waligusia kwa uchache suala la Wahadimu kwa kupinga kuwa hakuna Wahadimu bali kuna watu Wakae au Wamakunduchi (taz. Sengo, 1992; Chum, 1994; Iddi, 2011; Juma, 2011).

Pamoja na kujitokeza kwa kundi linalopinga suala la Wahadimu na Kihadimu, lakini bado tatizo liko pale pale; kwani hakuna utafiti wa kina uliofanywa wa kuthibitisha ukweli uliopo juu ya suala hili. Inaonekana kwamba pengine kundi hili limejiegemeza zaidi katika kuangalia eneo tu nakwamba Watumbatu wako Kaskazini na Wamakunduchi Kusini na hivyo labda haiwezi kuwa wote ni Wahadimu. Tumelazimika kujenga hoja hii kwa sababu pamoja na waandishi hawa kupinga kwamba hakuna Wahadimu, lakini hawakuweza kuonesha na kuthibitisha madai na shaka zilizopo. Hali hii imeendeleza kuwepo kwa kusigana na kukinzana kwa mitazamo hiyo.

Wamakunduchi ni watu wanaoishi Kusini mwa kisiwa cha Unguja, kama hivi ndivyo, bila ya shaka hawa ndio Wahadimu kwa vile wote wametajwa kuwa ndio wenyeji wa sehemu hiyo. Mbali ya makundi tuliyoyajadili hapo juu, baadhi ya wataalamu pia wamejaribu kuwahusisha Wamakunduchi na Wahadimu ambapo imedaiwa kuwa, jina hili lilianza kutumika wakati wa Wareno (taz. Werner, 1916). Madumulla (1995: 45-46), kinyume na wataalamu waliotangulia, anaeleza kuwa chimbuko la Wamakunduchi halifahamiki vizuri na hata hilo jina la Wamakunduchi ameliona likitajwa mara moja tu katika maandishi. Akiendelea kueleza na kuwanukuu Werner (1916) na Robinson, (1937), anasema wao wanadai kwamba jina kamili la Wamakunduchi ni Wahadimu. Kwa mujibu wa Werner jina la Wahadimu lilikuja katika kipindi cha Wareno, ambapo asili yao ni Winde katika sehemu ya Saadani huko Bagamoyo na watawala wao hadi kufikia mwishoni mwa karne ya 18 walikuwa ni Waarabu wenye asili ya Uajemi.

Tukirudi nyuma kidogo kwenye maelezo ya Madumulla aliyomnukuu Werner tutaona kuwa wanadai Watu hawa wanaoitwa Wahadimu walitoka Bagamoyo, labda tujiulize, je ndio wenyeji wa awali kufika katika maeneo ya Kusini? Je, kama ndivyo iweje wasubiri Waarabu hadi karne ya 18 ndio waje wawape jina? Au kabla ya hapo kulikuwa hakuna wenyeji wa asili katika

maeneo hayo?. Ama kwa hakika majibu ya masuali haya yanahitaji utafiti wa kina badala ya utashi wa mtu.

Kutokana na mitazamo tofauti tofauti iliyojitokeza kuhusiana na suala la Wahadimu, ni dhahiri kwamba hakuna utafiti wa kina si wa kihistoria tu, bali hata wa kiisimu uliofanywa kuhusiana na Wamakunduchi na Watumbatu.

**5.0 Hitimisho**

Katika kujadili suala la Wahadimu, tumeona wazi kwamba kuna mitazamo tofauti inayosigana na kukubaliana jambo linaloonesha kwamba utafiti zaidi kuhusu Wahadimu unahitajika. Aidha, pamoja na kutofautiana kwa mitazamo lakini wataalamu wanakubaliana kwamba neno hadimu limeletwa na Waarabu. Ama kuhusu maana ya neno hilo kumejitokeza wazi kwa tofauti ambapo; wataalamu wamelipokea na kulitafsiri katika miktadha tofauti, baadhi wanasema kuwa lina maana ya watumwa na wengine wakidai ni watumishi na manokoa. Pia, ingawa kuna kutofautiana kwa mitazamo juu ya Wahadimu, lakini takribani wataalamu wote wanakubaliana kuwa kabla ya kuja Waarabu katika visiwa vya Zanzibar walikuwapo wenyeji wa asili ijapokuwa kuna mkanganyiko katika kuwaeleza wenyeji hao walikuwa ni watu wa aina gani, jambo ambalo linahitaji kuchunguzwa zaidi kiisimu, kihistoria, kiakolojia na hata kiethnografia hasa ikizingatiwa kuwa maelezo yaliyopo hadi sasa ni changamani. Katika kufikia suluhisho la walau kujua kama Wahadimu walikuwapo ama laa, ni wenyeji wa asili ama laa, jee ni kweli waliishi Kusini na Kaskazini katika kisiwa cha Tumbatu ama laa; tafiti za kina zinahitajika. Kutokana na kusigana kwa mitazamo ya waandishi na wataalamu mbalimbali, makala haya yamejaribu tu kuonesha utata uliopo na kuchochea suala hili kuchunguzwa zaidi.

Pamoja na yote tuliyojadili kupitia mitazamo ya wataalamu tofauti, isidhaniwe kuwa makala haya yanadai kwamba hakuna Wahadimu, au Wahadimu hawakuwa watumwa au kinyume chake bali masuala yote haya yanahitaji kuchunguzwa kwa kina na uangalifu mkubwa.

## Marejeleo


Chami, F. A. (1994), *The Tanzanian Coast in the First Millenium AD: an archeology of the iron-working, farming communities*. Upsala: Societas Archeologica Upsaliensis.

__________ (2005), "The First Millenium AD on the East Coast: a new look at the cultural sequence and interactions". ktk *Azania XXIX-XXX* : 232 – 237.

__________ (2006), *The Unit of African Ancient History 3000 BC to AD 500.* Dar es Salaam: E & D Limited.

Chum, H. (1962/3), "A Vocabulary of the Kikae (Kimakunduchi, Kihadimu) Dialect". katika *Swahili: Journal of The East African Swahili Committee. vol 33/1:* 51-68. Dar es Salaam: East African Swahili Committee.

Davidson, B. (1967), *A History of East and Central Africa*. New York. Doubleday.

Freeman –Grenville, G.S.P. (1962), *The East African Coast: Selected Documents from the first to the earlier nineteenth Century*. London: Oxford University Press.

Gray, J.M. (1955), "Nairuzi or Siku ya Mwaka". ktk. *Tanganyika Notes and Records 38:* 1-22.

__________(1962), *A History of Zanzibar: From Middle Ages to 1856.* London.

__________ (1977), “The Hadimu and Tumbatu of Zanzibar”. katika *Tanganyika Notes and Records 81/82*: 135-53.

Hans, M. M. (2014), “Mchango wa Lahaja katika Kukuza na Kuendeleza Kiswahili Sanifu: Hazina Fiche Iliyomo katika Lahaja za Kiswahili za Zanzibar”. Tasinifu za Uzamivu (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Iddi, Z. A. (2011), “Phonological Processes in Kimakunduchi Dialect” Tasnifu za M.A (Linguistics) (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ingrams, W. H. (1924), “The Dialects of the Zanzibar Sultanate” in *Bulletin of the School of Oriental and African Studies, Vol.III, Part III,* London, pp 533-550.

__________ (1925), “The People of Makunduchi: Zanzibar”. Katika *Man.* Vol.25: uk. 138-142.

__________(1931), *Zanzibar: Its history and its people*. Repr. London: Cass 1967.

Johnston, H. H. (1922), *A Comparative Study of Bantu and Semi-Bantu Languages* (Juz.II). At the Clarendon Press: Oxford University Press.

Knappert, J. (1992), “A Short History of Zanzibar”. Katika *Annales Aequatoria.* Honore Vinek. Vol.13: uk. 15-37.

Madumulla, J.S. (1995), “Mwaka Kogwa [au Nairuz] katika Makunduchi”. Katika *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* Mlacha, S.A.K na Hurskainen, A (wah.). TUKI: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Makame, K. O. (2012), “Kirai Nomino katika Kitumbatu” Tasnifu za M.A (Kiswahili) (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Massamba, D.P.B. (2007), *Kiswahili Origins and The Bantu Divergence-Convergence Theory.*Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Studies.

__________ (2017), *Historia ya Kiswahili: Mtazamo Mpya 100KK hadi 2000BK.* Dar es Salaam: Kiswahili Development Ltd.

Prins, A.H. (1967): *The Swahili-Speaking Peoples of Zanzibar and the East African Coast (Arabs, Shirazi, and Swahili)*. London: International African Institute.

Robinson, A. E. (1937), “The Shirazi Colonization of East Africa”: katika *Tanganyika Notes and Records 3*: 40-80.

Saucleux, C. (1909), *Grammaire des Dialectes Swahili*, Paris.

Sendaro, A.M. (1997), *Slavery and Slave Trade.* Horizon Printing Services. Dar es Salaam.

Sengo, T.S.Y (1992), “Utamaduni wa Kiswahili: Wilaya ya Kusini Unguja.” Katika *Nordic Journal of African Studies*, Vol. 1/1. Helsink University Press.

Stigand, C. H (1915), *Grammar of Dialect Changes in the Swahili Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

__________ (1966), *The Land of Zinj*. London: Frank Cass & Co. Ltd.

Werner, A. (1916): “The Wahadimu of Zanzibar”. ktk. *Journal of African Society 15*: 325-60.